**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 7, Issue 1, 2024**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Mwingilianomatini kama Upekee wa Mtindo wa Emmanuel Mbogo: Mifano Kutoka Ngoma ya Ng'wanamalundi na Fumo Liongo

*Hadija Jilala*[1*]

[1] Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, S. L. P. 23409 Dar es Salaam, Tanzania.
[*] Barua pepe ya mawasiliano: dijaah@yahoo.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1770**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*22 Februari 2024*

**Istilahi Muhimu**:

*Mwingilianomatini, Mtindo, Upekee, Matini.*

## IKISIRI

Makala haya yanahusu mwingilianomatini kama upekee wa mtindo wa Emmanuel Mbogo kwa kurejelea tamthiliya zake mbili: Ngoma ya Ng'wanamalundi (1988) na Fumo Liongo (2009). Lengo la Makala haya ni kuibua upekee wa kimtindo wa Emmanuel Mbogo kupitia matumizi ya mwingilianomatini kwa kuangazia tamthiliya zake mbili alizoandika kwa kupishana muongo mmoja. Data zilikusanywa kwa kutumia mbinu mbili za ukusanyaji data ambazo ni usomaji makini na usaili. Aidha, nadharia ya mwingilianomatini imetumika katika kuchambua na kujadili data. Makala haya yanajadili kuwa matumizi ya mwingilianomatini katika utunzi wa Emmanuel Mbogo yanadhihirisha upekee wake wa kimtindo katika utunzi wake. Hili linajidhihirisha katika matumizi ya hadithi, ngoma, nyimbo, majigambo, wahusika wa fasihi simulizi, ushairi na nguvu za sihiri. Hivyo, makala haya yanahitimisha kuwa kila mtunzi ana upekee wake katika utunzi na uandishi wa kazi za fasihi, upekee huu hujidhihirisha katika uteuzi wa mtindo ambao unajirudiarudia katika kazi zake.

**APA CITATION**

Jilala, H. (2024). Mwingilianomatini kama Upekee wa Mtindo wa Emmanuel Mbogo: Mifano Kutoka Ngoma ya Ng'wanamalundi na Fumo Liongo. *East African Journal of Swahili Studies*, *7*(1), 98-113. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1770.

**CHICAGO CITATION**

Jilala, Hadija. 2024. "Mwingilianomatini kama Upekee wa Mtindo wa Emmanuel Mbogo: Mifano Kutoka Ngoma ya Ng'wanamalundi na Fumo Liongo". *East African Journal of Swahili Studies* 7 (1), 98-113. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1770.

**HARVARD CITATION**

Jilala, H. (2024) "Mwingilianomatini kama Upekee wa Mtindo wa Emmanuel Mbogo: Mifano Kutoka Ngoma ya Ng'wanamalundi na Fumo Liongo", *East African Journal of Swahili Studies*, 7(1), pp. 98-113. doi: 10.37284/jammk.7.1.1770.

**IEEE CITATION**

H. Jilala "Mwingilianomatini kama Upekee wa Mtindo wa Emmanuel Mbogo: Mifano Kutoka Ngoma ya Ng'wanamalundi na Fumo Liongo", *EAJSS*, vol. 7, no. 1, pp. 98-113, Feb. 2024.

**MLA CITATION**

Jilala, Hadija. "Mwingilianomatini kama Upekee wa Mtindo wa Emmanuel Mbogo: Mifano Kutoka Ngoma ya Ng'wanamalundi na Fumo Liongo". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 7, no. 1, Feb. 2024, pp. 98-113, doi:10.37284/jammk.7.1.1770.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1770

## UTANGULIZI

Dhana ya mwingilianomatini iliasisiwa na kuanza kutumiwa kwa mara ya kwanza na Mwanasemiotiki wa Kifaransa Julia Kristeva katika Makala yake ya *Word, Dialogue and Novel* (1966) na kisha ikajitokeza katika Makala yake ya *The Bounde Text* (1966-67). Kristeva alibuni dhana hii kwa kutumia na kuhusisha nadharia ya Semiotiki ya De Saussure na nadharia ya Usemezano ya Mikhail Bakhtin. Dhana ya Mwingilianomatini iliendelezwa na Bakhtin (1984) na Fairclough (1992) na hatimaye iliendelea kutumiwa na wanazuoni kama vile Allen (2000), Lemaster (2012), Wamitila (2003), Wamitila (2008), Senkoro (2011), Herman (2011) na Macha (2013). Wazo kuu la Kristeva katika Mwingilinomatini anasisitiza kwamba hakuna matini yoyote ya kifasihi inayoweza kujitegemea bila kuhusiana na matini nyingine. Uhusiano huu unaweza kuwa katika mtindo wa kiuashiriaji kama vile tashibiha na sitiari, dhamira, muundo wa msuko na usawiri wa wahusika. Msanii hutunga matini yake kutokana na matini za awali (Kristeva, 1978). Kwa hiyo, mwingilianomatini ni kuathiriana, kuhusiana na kutegemeana kwa kazi za fasihi, ambapo matini za kifasihi huingiliana na kuchangizana ili kukamilishana. Kristeva anasisitiza kuwa si rahisi kuzungumzia uasili au upekee wa kazi ya fasihi, kwani kwa vyovyote vile itakuwa imetokana na kazi za fasihi zilizotangulia au zilizopo. Hivyo, kuamini kuwa matini ya kifasihi inajitegemea ni kupotoka.

Allen (2000) na Lemaster (2012) wanakubaliana na mawazo ya Kriteva ambapo wanauona mwingilianomatini katika fasihini kuwa ni pale ambapo kitabu kimoja kinarejelea kitabu kingine katika jina la kitabu, visa na matukio, wahusika na usimuliaji. Vilevile, mwingilianomatini ni pale ambapo matini mbalimbali zinatumiwa ndani ya matini ya kifasihi kama vile, matumizi ya matini za kijamii, wimbo, hadithi za kitamaduni, filamu, maonesho ya televisheni na matini za vyombo vya habari.

Kwa upande wa fasihi ya Kiswahili, dhana ya mwingilianomatini imejadiliwa na wataalam mbalimbali, baadhi yao ni Wamitila (2003), Wamitila (2008), Senkoro (2011), Herman (2011) na Macha (2013). Wamitila (2008) anaeleza kuwa mwingilianomatini ni kule kuhusiana kwa kazi moja ya fasihi na kazi nyingine zilizotangulia. Mwingilianomatini huweza kuwa katika dhamira, wahusika, au mtindo.

Senkoro (2011) anafafanua mwingilianomatini kuwa ni kule kutumiwa kwa utanzu mmoja wa fasihi katika kutolea au kuwasilishia utanzu mwingine. Mfano, wimbo ndani ya ngano au hadithi. Halikadhalika, yaweza kuwa ni uwepo wa sifa mbalimbali za matini moja au zaidi katika kazi fulani ya fasihi, mfano, matumizi ya nyimbo, barua, ngoma, masimulizi ya hadithi, misemo, na nahau. Akiunga mkono hoja hii Macha (2013), anaeleza kuwa, mwingilianomatini ni ule uwepo wa sifa mbalimbali za matini moja katika kazi fulani ya fasihi, kama vile matumizi ya nyimbo, barua, ngoma, masimulizi ya dhati ndani ya hadithi, misemo, nahau, majibizano, vicheko na picha. Hivyo, wataalamu wote wanakubaliana kuwa mwingilianomatini ni kuhusiana na kukamilishana kwa kazi moja ya fasihi na kazi nyingine. Ufafanuzi na maelezo yao hayana tofauti na mawazo ya muasisi wa dhana hii Kristeva (1980) ambaye anauona mwingiianomatini kuwa ni kule kuathiriana, kuhusiana na kutegemeana kwa kazi za fasihi, ambapo matini za kifasihi huingiliana na kuchagizana ili kukamilishana. Kwa mujibu wake si rahisi kuzungumzia uasili au upekee wa kazi ya fasihi, kwani kwa vyovyote vile itakuwa imetokana na kazi za fasihi zilizotangulia au zilizopo. Hivyo, kuamini kuwa matini ya kifasihi inajitegemea ni kupotoka. Hapa tunajiuliza je mwingilianomatini ni upekee wa kimtindo wa Emmannuel Mbogo? Je, kazi zake zimetokana na kazi ipi ya fasihi?

Hivyo, baada ya kusoma kazi za fasihi zilizotungwa na Emmanuel Mbogo tuliona kuna matumizi ya mwingilianomatini. Aidha, kupitia kazi hizo yapo maswali ambayo tulijiuliza kuhusu utunzi wa Emmanuel Mbogo na matumizi ya mwingilianomatini. Maswali hayo ni: Je, matumizi ya mwingilianomatini ni upekee wa kimtindo wa Emmanuel Mbogo? Je, matumizi ya

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1770

mwingilianomatini yanayojitokeza katika kazi zake za fasihi yanadhihirisha upekee wake wa kimtindo? Kwa ujumla, maswali haya yalichochea utafiti na uandishi wa makala haya hasa baada ya kusoma kazi zote mbili na kubaini uwepo wa matumizi ya mwingilinomatini na pia baada ya kusoma tafiti zingine zilizofanywa kuhusu Emmanuel Mbogo hususan Mningo (2015).

## NADHARIA YA MWINGILIANOMATINI

Nadharia ya Mwingilianomatini ni nadharia ya uhakiki na njia ya kutafsiri matini ambayo iliasisiwa na Mwanasemiotiki wa Kifaransa, Julia Kristeva mwaka 1966. Chimbuko la nadharia hii ni mawazo ya nadharia ya de Saussure ya kiisimu ya Semiotiki na nadharia ya Usemezano ya Mikhail Bakhtin ambayo yalimfanya Kristeva kuja na nadharia ya Mwingilianomatini (taz. Moi, 1986; Worton na Still, 1990).

Katika kazi yake, '*A semiotic approach to Literature and Art'* (1969) Kristeva alijihusisha na kutambua jinsi matini inavyobuniwa na matini zilizopo. Anadai kuwa waandishi hawabuni matini kutokana na fikra zao ila hukusanya mawazo kutoka kwa matini zilizopo. Kwa hiyo, matini ni ugeuzaji taratibu wa matini au mwingilianomatini katika nafasi ya matini maalum. Anaeleza kuwa matini si kitu binafsi ila mkusanyiko wa matini za kitamaduni. Kristeva aliamini kuwa matini maalum na matini ya kitamaduni hubuniwa kutokana na malighafi sawa za kimatini ambazo haziwezi kutenganishwa.

Nadharia ya Mwingilianomatini inadai kuwa hakuna matini yoyote ya kifasihi inayoweza kujitegemea bila kuhusiana na matini nyingine. Uhusiano huu unaweza kuwa katika mtindo wa kiuashiriaji kama vile tashbihi na sitiari, dhamira, muundo wa msuko na usawiri wa wahusika (Wamitila, 2002).

Vilevile Nadharia ya Mwingilianomatini hii inadai kuwa kazi ya fasihi ina sauti mbalimbali zinazoingiliana na kupiga mwangwi katika kazi nyingine zilizotangulia, zilizopo, au zitakazokuja baadaye. Hii ina maana kwamba, athari ya kazi moja huweza kuonekana katika kazi nyingine zilizotangulia, zilizopo na hata zijazo. Kwa hiyo, hakuna matini yoyote inayoweza kuangaliwa peke yake, kwa upekee wake, na kwa kujitegemea, isipokuwa lazima kutakuwa na matini nyingine iliyotangulia ambayo inahusiana na matini hiyo mpya. Hii ina maana kwamba, kuna uhusiano na kutegemeana kwa kazi za fasihi, na kwa maana hiyo, si rahisi kuzungumzia uasili au upekee wa kazi ya fasihi, kwani kwa vyovyote vile itakuwa inatokana na kazi za fasihi zilizotangulia au zilizopo (Kristeva,1966; Jilala, 2016).

Nadharia ya Mwingilianomatini inasisitiza kuwa matini zinaingiliana na kuchangizana, hivyo kuamini kuwa matini ya kifasihi inajitegemea ni kupotoka. Pamoja na hayo mwingilianomatini huhusisha pia mitindo fulani ya kiusemi na misimbo fulani ambayo imesaidia katika uashiriaji wa kazi za baadaye. Hivyo mwingilianomatini sio urejelezi wa kazi fulani katika kazi nyingine tu, bali pia ni ule uingiliano wa mitindo ya kiuashiriaji (Kristeva, 1986).

Kristeva vilevile anataja kuwa muingiliano matini humaanisha kuweka 'historia katika matini na matini katika historia'. Anaeleza kuwa kuweka "historia katika matini" kuna maana kuwa matini huhusisha na hujengwa kutokana na matini za awali kwani matini ni sehemu muhimu ya historia. Kuweka "matini katika historia" kuna maana kuwa matini hujengwa upya, hutilia mkazo na ni mwangwi wa matini za awali hivyo hujenga historia na kuchangia mabadiliko mengi katika matini vilevile zikitazamia kujenga matini za baadaye (Kristeva, 1986).

Hivyo, mihimili na mawazo ya Nadharia ya mwigilianomatini ilituongoza katika kuchunguza, kujadili, na kutoa majumuisho ya malengo ya utafiti huu. Kupitia mihimili hiyo tuliweza kubaini vipengele vya mwingilianomatini katika kazi za Emmanuel Mbogo na jinsi mbinu hii inavyotumika kudhihirisha upekee wa kimtindo wa Emmanuel Mbogo katika utunzi na uibuaji wa dhamira za kazi zake za fasihi.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

## METHODOLOJIA

Data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia mbinu mbili ambazo ni; mbinu ya usomaji makini na mbinu ya usaili. Mbinu hii iliambatana na usomaji na uchambuzi wa matini za *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo*. Mchakato huu ulifanyika ili kupata data zinazohusiana na mwingilianomatini. Vilevile, mbinu hii ilihusisha usomaji, uchambuzi, na uchunguzi wa data katika vitabu na majarida yanayohusiana na mada ya utafiti huu, kama vipeperushi, taarifa za kwenye mtandao, na makavazi. Kwa kutumia mbinu ya usaili mtafiti aliweza kumhoji Mtunzi ili kupata data zaidi zinazohusiana na utunzi wake na matumizi ya mwingilianomatini katika kazi zake. Kwa ujumla mbinu zote mbili zilitumika kwa kujazilizana na kukamilishana.

## MATUMIZI YA MWINGILIANOMATINI

Lengo mahususi la makala haya lilikuwa ni kubainisha matumizi ya mwingilianomatini katika tamthiliya za *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (1988) na *Fumo Liongo* (2009) zilizotungwa na Emmanuel Mbogo kwa kupishana muongo mmoja. Hivyo, kupitia mbinu ya usomaji makini utafiti huu ulibaini kuwa tamthilia zote zinadhihirisha matumizi ya mwingilianomatini kama mbinu ya kimtindo. Matini ambazo zilibainishwa katika tamthiliya hizo ni kama zinvyojidhihirisha katika jedwali namba 1 hapa chini.

**Jedwali 1: Matumizi ya Mwingilianomatini**

| Na. | Aina ya matini | Fumo Liongo | Ngoma ya Ng'wanamalundi |
|---|---|---|---|
| 1 | Ushairi | ✓ | ✓ |
| 2 | Nyimbo | ✓ | ✓ |
| 3 | Ngoma | ✓ | ✓ |
| 4 | Nguvu za Sihiri | ✓ | ✓ |
| 5 | Majigambo | ✓ | ✓ |

**Chanzo**: Data za Utafiti Matini Teule (Juni, 2022)

*Jedwali 1* hapo juu linawasilisha matini ambazo zimetumika katika tamthiliya teule. Mtunzi anatumia mtindo wa ushairi, nyimbo, ngoma, nguvu za sihiri, na majigambo. Ujitokezaji wa matini hizo unadhihirisha kuwa mtunzi hutumia vipengele vya mwingilianomtini kama malighafi za kisanii katika utunzi wake. Hii inathibitisha kuwa mtunzi anatumia mwingilianomatini kama kipengele cha kimtindo kinachodhihirisha upekee wake wa utunzi na ubunifu wa kazi zake za fasihi. Sehemu ifuatayo inajadili ujitokezaji wa vipengele vya kimtindo kama mbinu za mwingilianomatini katika tamthiliya hizo.

### Matumizi ya Hadithi

Kwa mujibu wa TUKI (2013), hadithi ni habari za mambo yaliyotokea, mtungo wa habari, kisa, ngano, masimulizi, na hekaya. Utafiti huu ulibaini kuwa Emmanuel Mbogo katika utunzi wake ametumia hadithi alizopokea kutoka katika masimulizi ya visakale. Kwa mfano, katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi,* mtunzi ametumia masimulizi ya hadithi mbili ambazo ni: kisa cha Ubena Zomozi na kisakale cha Mwanamalundi kutoka katika kabila la Wasukuma. Hii pia inathibitishwa na mtunzi wakati wa usaili ambapo alikiri kuwa utunzi wa tamthiliya hii ni matokeo ya athari ya kazi tangulizi za fasihi simulizi ambazo alisimuliwa na kisha kutumia matini hizo kutunga tamthiliya hiyo kwa kutumia ubunifu na mbinu za kisanii.

Kisakale cha Mwanamalundi kinahusu mtu maarufu, shujaa na mwenye miujiza. Masimulizi ya kisakale hicho cha Wasukuma, imewahi kuandikwa na Boaz (1974). Mwanamalundi alizaliwa mwaka 1892 katika Wilaya ya Kwimba mkoani Mwanza. Alikuwa mcheza ngoma hodari, mwenye uwezo wa kufanya miujiza kutokana na dawa alizopewa na bibi kizee aliyekuwa ni mganga maarufu. Kwa mfano, alikuwa na uwezo wa kukausha miti iliyokuwa karibu yake kwa kuinyooshea kidole au kuishika, alikuwa na hirizi ambayo pindi anapoitupa baharini, maji hujitenga na kuacha nchi kavu katikati kama njia iliyomwezesha yeye na kijakazi wake kupita

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1770

katikati ya bahari kutoka sehemu moja kwenda ng'ambo ya pili (Mningo, 2015).

Kisakale kingine ambacho mtunzi alikitumia kama malighafi ni masimulizi ya kisa cha kweli cha Ubena Zomozi. Wakati wa usaili, mtunzi anaeleza kuwa alikwenda katika Kijiji cha Ubena Zomozi kumtembelea rafiki yake. Akiwa hapo aliona baadhi ya nyumba zimebomolewa, na miongoni mwa nyumba hizo ni nyumba ya mzee mmoja aliyekuwa anamfahamu. Rafiki yake alimueleza kuwa mzee huyo alihama kijiji hicho kwa sababu ya aibu baada ya kufichuliwa kuwa ni mchawi anayefuga misukule na watu wanaojiita Konikoni, ambao hufichua wachawi kwa nguvu ya dawa zao. Aidha, ilibainika kuwa misukule hao walikuwa wanatumikishwa na mzee huyo kwa kumzalishia mali, kumlimia mashamba na shughuli nyinginezo. Kwa hiyo, baada ya kupata masimulizi haya mtunzi anaeleza kuwa yalimvutia na kisha alipata wazo la kuandika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi*, tamthiliya ambayo inajadili dhamira mbalimbali zinazojitokeza katika jamii kama vile matabaka, utumikishaji, ukandamizaji na unyonyaji.

Hivyo, katika utunzi wa tamthiliya hiyo, mtunzi amechukua sifa za Mzee wa Ubena Zomozi za uchawi na ufugaji wa misukule na kuzitumia kumjenga mhusika mkuu wa tamthiliya yake "Chidama". Msanii anajenga taswira ya kisanaa ambayo inawakilisha Chidama na misukule anaowatunza baada ya kuwaua kwa njia ya uchawi. Kupitia mtindo huu, msanii anaibua uovu ambao unafanyika ndani ya jamii. Mhusika Chidama amechorwa kama mtu wa tabaka tawala ambalo linafanya kazi ya uonevu, unyanyasaji na ukandamizaji. Nguvu za uchawi alizopewa zinatumika kitaswira kuashiria uwezo na madaraka anayokuwa nayo mtu na kuyatumia kwa kutumia mbinu mbalimbali ili kukandamiza tabaka la wanyonge. Kitendo cha Chidama kutumia uchawi kuharibu ubongo wa watu kwa kutumia uchawi ili kuwaweka katika milki yake na kuwatawala ni mbinu ya kitaswira ambayo inadhihirisha uhalisia wa mbinu zinazotumiwa na watawala wa tabaka tawala dhidi ya wanyonge. Hivyo, msanii anaibua dhamira zake kupitia taswira na ishara zinazojengwa kutokana na athari ya masimulizi ya kisa cha kweli cha Ubena Zomozi. Katika tamthiliya hii, msanii ametumia matini ya hadithi ya kweli kujenga ukweli wa jamii kisanii kwa kuhamisha ukweli wa masimulizi na kuuweka katika mtindo wa kisanii ili kuibua dhamira ndani ya jamii.

Vilevile, msanii ametumia sifa na jina la Mwanamalundi wa kisakale cha jamii ya Wasukuma na kumuumba mhusika Ng'wanamalundi katika tamthiliya ili kujenga taswira ya ukombozi na harakati za mapinduzi ya kijamii. Mwanamalundi kama ilivyo katika kisakale cha Ng'wanamalundi ni shujaa, jasiri na mtu maarufu sifa hizi zinahamishiwa kwa mhusika wa tamthiliya, ambapo anajengwa kwa kupewa sifa ya shujaa, mwelimishaji, jasiri, mpenda haki na usawa anayeongoza mapinduzi kwa kuwasaidia vizuu kukomboa mali zao kutoka kwa Chidama na kuzirudisha mikononi mwao. Pia amepewa sifa ya kuwa mganga maarufu anayepambana na udharimu wa Chidama na himaya yake.

Utafiti huu umebaini kuwa dhana ya ukombozi, kupigania haki, usawa na mali zilizodhurumiwa na viongozi wenye sifa ya ukandamizaji na unyonyaji inajengwa kupitia taswira ya kisakale cha Ng'wanamalundi wakati dhana ya unyonyaji, ukandamizaji na udhalimu inajengwa kupitia kisa cha Mzee wa Ubena Zomozi. Mtindo huu ambapo msanii anaunganisha matini mbili zenye taswira tofauti za nguvu ya uchawi na nguvu ya uganga ili kujenga matabaka ya walionacho na wasio nacho, wakandamizaji na wapigania uhuru.

Hivyo, mawazo na mihimili ya nadharia ya mwingiliano matini unajidhihirisha katika utunzi wa tamthiliya hii. Kupitia mbinu ya uhamishaji na utumizi wa sifa za wahusika kutoka katika visakale vyote viwili na kuzihamishia kwa wahusika wa tamthiliya zake inadhihirisha msingi wa nadharia ya mwingilianomatini ambao unasema kuwa mtunzi huchota matini za kazi moja ya fasihi na kuihamishia katika matini nyingine ya fasihi (taz. Wamitila, 2003; Senkoro, 2011).

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1770

Athari ya mapokeo simulizi katika utunzi wa Emmanuel Mbogo inadhihirika katika tamthiliya ya *Fumo Liongo* ambapo matumizi na uteuzi wa majina ya wahusika na sifa wanazopewa ni matokeo ya mapokeo simulizi ya utendi wa "Fumo Liongo". Mhusika mkuu wa tamthiliya hiyo amepewa jina la Fumo Liongo anayezungumziwa katika utendi wa *Fumo Liongo*. Majina ya wahusika wengine kama vile; Mbwasho na Sada ni majina ya wahusika wanaojitokeza katika utendi wa *Fumo Liongo*.

**Matumizi ya Hadithi ndani ya Hadithi**

Utafiti huu ulibaini kuwepo kwa matumizi ya hadithi ndani ya hadithi kama matokeo ya athari ya mapokeo simulizi. Tazama mfano katika dondoo Na. 1.

> *"…Si mganga tu bali ni mtu wa ajabu. Alizaliwa kimiujiza na atajakufa kimiujiza. Ngano zinaeleza kuwa: baba yake Ng'wanamalundi aliambiwa na mganga wake kuwa utazaa mtoto mmoja tu wa kiume na wewe kama dume la nyuki, utaiaga dunia. Kweli. Mara baada ya mkewe kutunga mimba yake Ng'wanamalundi aliiaga dunia. Siku alipozaliwa Ng'wanamalundi mvua kubwa ya mawe ilinyesha nchi nzima. Mito ikafurika, radi za mvua zikachana na kuunguza mibuyu na mikuyu. Tetemeko la ardhi lilirindima toka mashariki ya dunia hadi magharibi. Na ghafla mchana wa jua la utosini ukakumbwa na giza nene. Lakini mkunga aliukata mnyororo wa kitovu cha mtoto yule mchanga, akakirusha juu! Kikapaa kikanata mawinguni – na akakirusha juu! Kikapaa kikanata mawinguni – Na tazama: ghafla giza likatoweka na jua likaangaza tena katikati ya upindi wa mvua…."* (Uk. 27-28)

Chanzo: Data za Utafiti kutoka Kitabu Ngoma ya Ng'wanamalundi (Juni, 2022)

Dondoo hiyo inaonesha kuwa mtunzi ametumia hadithi ndani ya hadithi kwa kutumia mtindo wa usimulizi wa hadithi za kijadi kuelezea safari ya mazazi ya Ng'wanamalundi, maisha yake na kazi yake. Mtunzi anatumia hadithi kama mbinu ya kimtindo kutokana na athari aliyoipata kutoka kwenye kisa cha Ng'wanamalundi.

Mbinu hii ni muhimu kwa sababu inamsadia mtunzi kuibua dhamira na kuelezea matukio yaliyopo ndani ya jamii. Hivyo, kutokana na data hizo tunaweza kusema kuwa tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* ni matokeo ya athari ya masimulizi ya kimapokeo ya kisakale cha Wasukuma na masimulizi ya tukio la kweli la Ubena Zomozi ambavyo kwa pamoja vilimuathiri mtunzi na kisha kutumia sanaa na ubunifu wa kifani na kimaudhui kwa kuchota maudhui toka katika masimulizi hayo na kuleta uhusiano wa kimaudhui na wahusika baina ya masimulizi hayo na tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi*. Ubunifu huu wa kuchota malighafi za kutungia tamthiliya kutoka katika masimulizi ya kweli yaliyowahi kutokea katika jamii, unaonyesha upekee wa kimtindo wa Emmanuel Mbogo.

**Matumizi ya Utendi**

Mulokozi (1996) anafasili tendi kama utungo wenye kusimulia matukio ya kishujaa katika ngazi ya kijamii au kitaifa. Matukio yanayosimuliwa huweza kuwa ya kihistoria au huchanganya na visakale au visasili. Utafiti huu umegundua kuwa, tamthiliya ya *Fumo Liongo* ni matokeo ya mwingilianomatini ambapo mtunzi aliathiriwa na mapokeo simulizi ya utendi wa "Fumo Liongo" na hivyo kutunga tamthiliya ya *Fumo Liongo*. Utendi huu unaelezea mambo yaliyowahi kutokea katika historia ya mji wa Pate. Utendi huo uliandikwa mwaka 1913 na Muhamadi bin Abubakar bin Omari al-Bakry aliyejulikana zaidi kwa jina la Muhamad Kijumwa. Inasadikiwa kuwa Kijumwa aliandika utendi huo baada ya kupata hadithi ya mapokezi simulizi yanayomhusu mtu maarufu katika historia ya Pate, aliyeitwa Fumo Liongo, anayeaminika kuwa aliishi katika karne ya 13 hadi 14, (TUKI, 1999).

Kwa ujumla, utendi wa "Fumo Liongo" unaelezea mgogoro uliokuwepo kati ya Fumo Liongo na kaka yake Mfalme wa Pate aliyeitwa Daudi Mringwari. Mgogoro huo ulitokana na hofu iliyokuwa imemtawala mfalme Daudi Mringwari, kuhusu kunyang'anywa ufalme wake na nduguye

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1770

Fumo Liongo, ambaye alitokea kuwa mwenye nguvu, shujaa, jasiri, manju na malenga hodari aliyependwa na wananchi wa Pate. Hofu hiyo ya mfalme ilijenga chuki na fitina kali dhidi ya Fumo Liongo, kiasi cha mfalme kutafuta mbinu mbalimbali za kutaka kumuua. Fumo Liongo aligundua mipango hiyo ya ndugu yake ya kutaka kumuua, akaamua kuondoka Pate na kwenda kuishi nyikani na Wasanye, Wadahalo, Waboni na Watwa.

Utafiti huu ulibaini kuwa, mapokezi simulizi ya hadithi ya utendi huo, yanafanana kwa kiasi kikubwa na tamthiliya ya *Fumo Liongo.* Hii inadhihirisha kuwa mtunzi aliathiriwa na mapokeo simulizi ya utendi huo katika kutunga tamthiliya ya *Fumo Liongo*. Vilevile Emmanuel Mbogo wakati wa usaili alikiri kuathiriwa na masimulizi hayo ambayo yalimsukuma kutunga tamthiliya ya Fumo Liongo. Wamitila (2003) anaeleza kuwa, kazi za fasihi huathiriana kiasi cha athari hizo kuonekana moja kwa moja katika kazi nyingine ya fasihi, hata kama watunzi wake ni tofauti na wana uzoefu tofauti. Vilevile kufanana huko kunadhihirisha mawazo ya Kristeva (1960) katika nadharia yake ya mwingilianomatini inayoeleza kuwa, katika kazi za fasihi kuna kuhusiana na kutegemeana, hivyo si rahisi kuzungumzia uasili au upekee wa kazi ya fasihi, kwani kwa vyovyote vile itakuwa inatokana na kazi za fasihi zilizotangulia au zilizopo.

Utafiti huu ulibaini kuwa mtunzi amehamisha matukio yaliyomo katika Utendi wa “Fumo Liongo” na kuyatumia katika utunzi wa tamthiliya ya *Fumo Liongo*. Athari hii inajidhihirisha katika kisa cha Wagala kutaka mbegu ya Fumo Liongo katika kabila lao. Tazama dondoo Na. 2:

> *ZAHIDI: Mama ana mtoto.*
>
> *MBWASHO: Nimesikia. Mtoto gani baba?*
>
> *LIONGO: Madi unakumbuka mwaka jana ulipokuja ule ujumbe wa Mfalme wa Gala kumwomba Mringwari nikubali kutoa mbegu ya simba?*
>
> *MADI: Nakumbuka sana.* Uk 17

Chanzo: Data za Utafiti katika *Fumo Liongo* (Juni, 2022)

Mfano katika dondoo namba 2 nadhihirisha mwingilianomatini wa matumizi ya kisa kilichopo kwenye utendi kwenda kwenye tamthiliya. Mfano ni kisa cha Wagala walivyohitaji mbegu ya Fumo Liongo kwa ajili ya vizazi vyao kutokana na ujasiri, ushujaa, ushupavu na matendo yake. Sifa hizi zinajitokeza katika matumizi ya sitiari ‘simba’ iliyotumika kumrejelea Fumo Liongo. Kisa hiki kinajitokeza pia katika Utendi wa “Fumo Liongo” ambapo Wagala wanaomba wapatiwe mbegu ya Fumo Liongo ili apate kuwazalia watoto wenye sifa kama zake. Kisa hicho kinapatikana katika utendi wa “Fumo Liongo” ubeti wa 41. Tazama dondoo na. 3.

> *“Twaitaka mbeu yake*
>
> *nasi kwetu tuipeke*
>
> *kwa furaha tumuweke*
>
> *apate kutuzaliya”.* Uk 29

Chanzo: Data za utafiti katika *Tenzi Tatu za Kale* (Juni, 2022)

Katika dondoo namba 3 hapo juu tunaona jamii zingine zikihitaji kupata mbegu ya Fumo Liongo hili pia linajitokeza katika tamthiliya ya *Fumo Liongo*. Hii inadhihirisha kuwa mtunzi aliathiriwa na utendi huo kifani na kimaudhui. Vilevile, utafiti huu ulibaini kuwa mtunzi anatumia pia mbinu na mtindo wa kisanii katika kuwasilisha maudhui hayo mfano ni matumizi ya sitiari ‘simba’ katika tamthiliya yake.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Mwingilianomatini, utunzi wa aina hii unadhihirisha uathiriano na uhusiano wa matini za kifasihi. Kwamba mbinu za uteuzi wa matini za kifasihi hutokana na muathiriano wa kazi za kifasihi zilizotangulia na kusaidia katika uashiriaji wa kazi za baadaye.

**Matumizi ya Ngoma**

Utafiti huu ulibaini kuwa mtunzi ametumia ngoma katika tamthiliya zake zote mbili. Kwa mfano, katika *Ngoma ya Ng’wanamalundi*

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1770

matumizi ya 'Ngoma' yanadhihirisha mwingilianomatini. Utafiti huu ulibaini kuwa Msanii amechota mbinu ya matumizi ya ngoma kutoka katika kisakale na kuingiza katika utunzi wake. Kupitia usomaji makini, tulibaini kuwa dhana ya ngoma katika tamthiliya ya Ngoma ya Ng'wanamalundi imetumika kisitiari na inajidhihirisha kwa namna tatu: kwanza ni ngoma ya harusi, pili ni ngoma ya chidama, na tatu ni ngoma ya Ng'wanamalundi.

Hivyo, matumizi ya ngoma yanadhihirisha mwingilianomatini unaotokana na athari ya matumizi ya ngoma katika kisakale cha kabila la Wasukuma kuhusu shughuli ya kucheza ngoma za asili aliyokuwa anaifanya Ng'wanamalundi. Mtunzi anaitumia ngoma kisitiari ili kuibua dhamira za ujenzi wa jamii mpya na nafasi na wajibu wa vijana katika ujenzi wa jamii mpya na mapambano ya kutafuta uhuru wa kweli. Hivyo, sifa, kazi, na matendo ya Ng'wanamalundi katika kisakale yameathiri utunzi na ubunifu wa Emmanuel Mbogo.

Matumizi ya ngoma yanajitokeza pia katika tamthiliya ya *Fumo Liongo*. Katika tamthiliya hii ngoma imetumika kama ishara ya furaha na hili linajidhihirisha wakati wananchi wa Pate walipofanya sherehe ya kumpokea shujaa Fumo Liongo alipokuwa akirejea kutoka kwenye vita vya kuikomboa nchi yao dhidi ya uvamizi wa *Wabuu* wa Sango Vere. Tazama dondoo na. 4:

> *MKE: Hao! (Anaruka) Hao! Mume wangu, hao! (Anapiga vigelegele huku akifunga kibwaya chake vizuri). Sikubali! Nakwambia sikubali. Leo na miye nitapenya lufufu ya watu hadi niyaguse manyoya ya Simba wa Pate… (Anaimba wimbo wa kumsifu Liongo wakati huohuo wanangoma wanaingia na wote wanacheza kwa pamoja)* uk. 3

Chanzo: Data za Utafiti katika *Fumo Liongo* (Juni, 2022)

Dondoo namba 4 hapo juu unadhihirisha dhima ya ngoma katika jamii ya Pate ambayo ni kuburudisha jamii. Utafiti huu ulibaini kuwa, matumizi ya ngoma ni matokeo ya athari ya mapokeo simulizi ya utendi wa "Fumo Liongo", katika utendi huo tunabainishiwa kuwa Fumo Liongo alikuwa ni manju na malenga stadi katika uimbaji na uchezaji ngoma. Haya yanadhihirishwa na ubeti wa 79 katika uk.35.

> *Liongo nikwambiao*
>
> *Shaha wa gungu na mwao*
>
> *tena ni mkuu wao,*
>
> *huwashinda wut'e piya*

Chanzo: Data za utafiti katika *Tenzi Tatu za Kale* (Juni, 2022)

Tukirejelea nadharia ya mwingilianomatini, inaaminika kuwa, matini huchukua au hufaidi kutokana na matini nyingine (Wamitila, 2002). Hii ina maana kwamba kuwepo kwa matini katika kazi ya fasihi ni kuwepo kwa matini nyingine katika kile kinachoitwa mwanda wa kimwingilianomatini, katika kukamilishana na kujengana ili kuleta maana.

**Mtindo wa Matumizi ya Nyimbo**

Katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi,* utafiti huu ulibaini kuwepo kwa mtindo wa matumizi ya wimbo kama mwingilianomatini. Tazama dondoo namba 6:

> *SECHE (anaimba)*
>
> *Leo mambo mtaona*
>
> *Leo mambo mtaona*
>
> *Tumembadili kijana!*
>
> *Tumembadili kijana!* Uk 5

Chanzo: Data za Utafiti (Juni, 2022)

Katika dondoo namba 6 hapo juu inadhihirisha matumizi ya wimbo katika tamthiliya ya Ngoma ya Ng'wanamalundi. Mtunzi ametumia matini za fasihi simulizi kama mbinu ya utunzi ili kuingiza ujumi wa Kiafrika na kutumia utajiri wa tanzu za fasihi simulizi kama mbinu za utunzi wa tamthiliya hii. Mutembei (2012), anaeleza kuwa

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1770

nyimbo zinazotumiwa katika kazi za fasihi za Kiafrika huwa ni sehemu ya kazi hiyo ya fasihi na huwa ni kipengele muhimu katika kujenga maana nzima ya simulizi katika kazi hiyo ndani ya kazi yenyewe. Hivyo, katika tamthiliya hii matumizi ya nyimbo ni mwingilianomatini unaodhihirisha kuathiriana na kuingiliana kwa tanzu za kifasihi katika mbinu za utunzi, kwa lengo la kuchangizana na kutegemeana ili kukamilishana kimaana, kama anavyobainisha Kristeva (1960) katika nadharia yake ya mwingilianomatini.

Katika Fumo Liongo, msanii pia ametumia wimbo. Mwandishi ametumia wimbo wa kumsifu Liongo baada ya kurejea kutoka vitani ambapo aliongoza mapambano dhidi ya Wabuu wa Sango Vere na kupata ushindi. Haya yanabainika katika mfano ufuataao.

> *MUME: Umesikia! (Akisisitiza.) Simama twende mwanamke! (Wanapita watu wanneama watano hivi wakiimba.) Liongo! Simba! Liongo! Simba! (Kisha wanatoka.)* Uk 1.

Chanzo: Data za Utafiti katika *Fumo Liongo* (Juni, 2022)

Mfano katika dondoo namba 7 hapo juu unadhihirisha matumizi ya wimbo katika matini ya tamthiliya ya Fumo Liongo. Matumizi ya wimbo pia yanajitokeza katika tukio la Liongo alipokuwa gerezani wakati akimpa Sada maagizo ya kumpelekea mama yake, Bi Mbwasho, ili amtengenezee mkate na katikati aweke tupa. Tazama dondoo namba 8 hapa chini:

> *LIONGO: Ebu imba tena nikusikie Kijakazi wangu mwema.*
>
> *SADA: (Anaimba.)*
>
> *Ewe Kijakazi na kutuma uwatumika,*
>
> *Kamwambie mama, ni mwinga siyalimika,*
>
> *Afanye mkate, kati tupa kuweka,*
>
> *Nikeze pingu na minyoo ikinyooka,*
>
> *Ningie ondoni ninyinyirikeja mana nyoka,*
>
> *Tatange madari na makuta kuno kumeta.* Uk 25 -26

Chanzo: Data za Utafiti katika *Fumo Liongo* (Juni, 2022)

Dondoo namba 8 hapo juu linadhihirisha matumizi ya wimbo. Nyimbo katika jamii za Afrika hutumika katika nyakati mbili; wakati wa furaha na wakati wa shida ama huzuni[1]. Hivyo, wimbo wa Liongo umetumika wakati wa shida. Vilevile, utafiti huu ulibaini kuwa, matumizi ya wimbo huo ni athari ya moja kwa moja ya utendi wa "Fumo Liongo" katika tamthiliya ya *Fumo Liongo*. Mwandishi ameuchukua wimbo huo kutoka katika utendi wa "Fumo Liongo" uk 58, na kuutumia katika utunzi wa tamthiliya yake. Tazama dondoo namba 9:

> *Ewe kijakazi nakutuma hujatumika*
>
> *Kamwambie mama ni muyinga hajalimuka*
>
> *Afanye mkate pale kati tupa kaweka*
>
> *Nikeeze pingu na minyoo ikaniuka*
>
> *Nitatage kuta na madari yakiyekuka*
>
> *Niuwe rijali wake wana nikiwateka*
>
> *Katokeze nde kama kozi nikatotoroka…* uk 58

Chanzo: Data za utafiti katika *Tenzi Tatu za Kale* (Juni, 2022)

Dondoo namba 9 hapo juu linaonesha wimbo unaojitokeza katika tamthiliya ya *Fumo Liongo* kuwa ni matokeo ya utendi wa *"Fumo Liongo"*. Wamitila (2002) anafafanua kuathiriana huko kwa kusema kuwa matini za awali zinasaidia uelewekaji wa kazi za baadaye. Hapa tunaona jinsi wimbo wa utendi ulivyosaidia uelewekaji maudhui ya tamthiliya hii.

[1] Wazo hili linajidhihirisha katika jamii za Kiafrika tunaona nyimbo zikiimbwa wakati wa sherehe, harusi, mikusanyiko ya furaha. Katika kipindi hiki nyimbo za kupongezana na kufurahiana huimbwa kwa furaha na vifijo Nyimbo pia huimbwa wakati wa msiba kwa ajili ya kuwaliwaza wafiwa na kumuombea marehemu na hata waliobaki.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1770

Halikadhalika, wimbo mwingine uliojitokeza ni ule wa maombolezo ambao uliodokezwa ukiimbwa, bila kuainishwa maneno yake. Wimbo huo unaimbwa na watu waliokuwa wamebeba maiti ya Fumo Liongo. Tazama dondoo namba 10:

*WATU: Motoooo!!! Choma Mringwari, uwa!... (Radi na ngurumo mvua…Sambamba wimbo wa maombolezo unasikika ukiimbwa taratibu…) uk 48*

Chanzo: Data za Utafiti katika *Fumo Liongo* (Juni, 2022)

Mfano huo unathibitisha kuwa matumizi ya wimbo ni matokeo ya athari ya fasihi simulizi ya Kiafrika na falsafa ya Kiafrika ambapo wimbo hutumika kama mbinu ya faraja kwa jamii iliyokumbwa na huzuni. Utafiti huu ulibaini kuwa, wimbo huu wa maombolezo umedokezwa tena na Machaka na Mwanamke, bila kubainishwa maneno yake baada ya mauaji ya watu yaliyofanywa na mazabania wa mfalme Mringwari uk 51. Tazama dondoo lifuatalo:

*Ila sasa wakati wa kuwakafini na kuwasitiri*

*Kwa maji ya machozi yetu Hawa waliolala sasa umewadia [anapiga rimba, akiimba wimbo wa maombolezo pamoja na mwanamke*

*Aliyekuwa analia…]*

Chanzo: Data za Utafiti katika *Fumo Liongo* (Juni, 2022)

Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa, wimbo wa maombolezo na ule wa kuburudisha katika sherehe za mapokezi ya Liongo kutoka vitani, zinatokana na ubunifu wa mtunzi, hazimo katika utendi. Hivyo mwandishi katika tamthiliya hii, ameonyesha dhima tatu za nyimbo ambazo ni kuburudisha, kuelimisha na kuombeleza. Hii imebainika kulingana na mazingira na matukio ambamo nyimbo hizo zimetumika. Wakati wa usaili, mtunzi alieleza kuwa matumizi ya nyimbo katika tamthiliya hii, yamekusudia kuingiza ujumi wa Kiafrika na kutumia utajiri ulioko katika fasihi simulizi ya Kiswahili.

**Mtindo wa Matumizi ya Majigambo**

Wamitila (2003) anafasili majigambo kuwa ni aina ya maghani (sifo) yanayohusu kujisifu au sifa, aghlabu kuhusu kutongoa utungo wa kujisifu kuhusiana na kitendo fulani cha ushujaa, urijali au matendo muhimu (tazama pia Samwel, 2012; Mulokozi; 1996). Katika makala haya, matumizi ya majigambo katika utunzi wa tamthiliya teule za Emmanuel Mbogo.

Aidha, utafiti huu ulibaini kuwa mbinu ya majigambo katika tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* inajidhihirisha katika nyanja mbili ambazo ni; majigambo ya tabaka tawala na mjigambo ya tabaka tawaliwa. Majigambo ya tabaka tawala yanawasilishwa na Chidama wakati akimtumia Ng'wanamalundi joka la vichwa saba, ili liende likamfundishe adabu na heshima. Tazama mfano ufuatao:

*CHIDAMA: Joka la vichwa saba*

*Lakini ni joka moja tu*

*moja katika saba na saba katika moja,*

*Ewe mtambaa chini,*

*Mwenye meno ya sumu*

*Mwenye kinywa kilichojaa*

*misumari na miiba ichomayo*

*na kurarua bila huruma…*

*Haya nawende, nakutuma:*

*Nenda ukatumbukize ukucha wako wa chuma ubavuni mwake,*

*Ukamfutue na kumfumua matumbo yake*

*Ukumzingire na kumzingara figo zake*

*Umkamue anye na kujinyea*

*Umminye akojoe na kujikolea.*

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1770

> *Ajue kuwa Chidama ni Chidama kweli*. Uk 15-16.

Chanzo: Data za Utafiti (Juni, 2022)

Dondoo namba 12 hapo juu inadhihirisha matumizi ya majigambo kama kipengele cha mwingilianomatini katika utunzi wa Emmanuel Mbogo. Utafiti huu ulibaini kuwa mtunzi amemtumia Chidama kisitiari kuwakilisha tabaka tawala lenye nguvu kiuchumi. Hivyo, mbinu ya majigambo imetumika kuonesha jinsi tabaka tawala linavyotumia uwezo na nguvu katika kupambana na harakati za ukombozi.

Vilevile, mtunzi ametumia majigambo ya tabaka tawaliwa yanayowasilishwa na shujaa anayejidhihirisha kama mtetezi wa wanyonge, Ng'wanamalundi. Tazama dondoo namba 13 hapa chini:

> *NG'WANAMALUNDI: Najua aliyekutuma*
>
> *Lakini huyo si mulume sawasawa.*
>
> *Wewe ni tonga, hujawa tui bado. Huchochote bali garasa, shushu la nyoka mgonjwa, (anamtemea mate yule nyoka).*
>
> *Lakini nakutambua wewe U nani.*
>
> *Najua ndiye wewe yule anukae damu ya maskini.*
>
> *Huwezi kunizuga na mavazi uliyovaa. Kwani sabuni na manukato havitoshi kutoharisha nuksi iliyoko ndani ya kichwa, roho na matendo yako. Kwani nani hajui kuwa wewe ni mchawi wa msukule?* (uk. 34)

Chanzo: Data za Utafiti (Juni, 2022)

Data katika dondoo namba 13 hapo juu inadhihirisha majigambo ya tabaka tawaliwa kupitia Ng'wanamalundi. Majigambo hayo yanadhihirisha uelewa wa jamii juu ya mbinu za tabaka tawala na kuwa haiwezi kushindana na harakati za mapinduzi. Hivyo, mbinu ya majigambo imetumika kisanii kuingiza ujumi wa Kiafrika katika kazi za sanaa na kuleta uhalisia wa maisha ya shujaa wa Kiafrika, ambaye huambatana na majigambo na kujisifu.

Katika Tamthiliya ya *Fumo Liongo*, matumizi ya mbinu ya majigambo pia yamejitokeza. Tazama dodondoo ifuatayo:

> *LIONGO: Unanijua mama, unanijua. Lakini wakati mwingine nadhani unanisahau: Unasahau kuwa mimi si mwanao tu bali pia mimi ni Liongo! Fumo Liongo Mama. Liongo Simba wa Pate ninayeweza kuunguruma na kuleta zilizala kwa watakao kunichezea, Liongo! Ala! He! …. Uk16.*

Chanzo: Data za Utafiti katika *Fumo Liongo* (Juni, 2022)

Mfano huo unaonesha majigambo ambayo mhusika Liongo anayatumia kujigamba juu ya uwezo na nguvu alizonazo kwa kutumia sitiari ili kuonesha sifa za shujaa wa Kiafrika. Hata hivyo, utafiti huu ulibaini kuwa mbinu hii ya majigambo haikujitokeza katika utendi wa Fumo Liongo bali ni mwingilianomatini ambao mtunzi anatumia mbinu za fasihi simulizi ya Kiafrika katika utunzi wa tamthiliya. Kwa kutumia ubunifu huu msanii anachota sifa za mhusika Fumo Liongo kutoka katika utendi wa "Fumo Liongo" na kutumia mbinu za kisanii kumvisha sifa hizo mhusika wa tamthiliya yake. Hii inatokana pia na mtunzi kuathiriwa na mapokezi simulizi kuhusu mashujaa wa Kiafrika.

## MATUMZI YA WAHUSIKA WA FASIHI SIMULIZI

Utafiti huu umebaini kuwa, mtunzi ametumia wahusika kutoka katika fasihi simulizi, mfano matumizi ya Joka la vichwa saba. Majigambo ya tabaka tawala yanawasilishwa na Chidama wakati akimtumia Ng'wanamalundi joka la vichwa saba, ili liende likamfundishe adabu na heshima. Rejelea mifano iliyotolewa katika dondoo namba 12.

### Matumizi ya Ushairi

Utafiti huu ulibaini kuwa, mbinu ya ushairi inajitokeza katika tamthiliya zote mbili. Mfano,

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1770

katika Ngoma ya Ng'wanamalundi msanii ametumia ushairi na kuuingiza kama mbinu ya utunzi wa tamthiliya yake. Tazama dondoo lifuatalo hapa chini:

*Ewe mtabaa chini*

*Ewe kifutu wangu, mfutua watu*

*Ewe chatu wangu, mvunja mbavu…* uk 15

Chanzo: Data za Utafiti (Juni, 2022)

Dondoo namba 15 hapo juu linadhihirisha matumizi ya mbinu ya mtindo wa ushairi kama kipengele cha mwingilianomatini. Mbinu hii ni miongoni mwa mbinu ambazo wakati wa usaili, msanii alizielezea kuwa alizitumia ili kuingiza vionjo vya fasihi simulizi ya Kiafrika katika utunzi wa tamthiliya.

Vile vile utafiti huu ulibaini kuwa, mtunzi anatumia nyoka kwa kumpa sifa za kibinadamu. Matumizi wahusika wa fasihi simulizi ni athari ya fasihi simulizi ya Kiafrika ambapo wanyama, mizimu, majoka, miti na mawe hutumika kama wahusika wa kazi za fasihi. Mbinu ya kutumia wahusika Wanyama kama ambavyo wanatumiwa katika fasihi simulizi inadhihirisha mwingilianomatini utanzu wa fasihi simulizi katika tamthiliya. Anatumia nyoka ili kujenga dhamira ya hatari na kujenga.

Matumizi ya mbinu ya mtindo wa ushairi inajitokeza pia katika tamthiliya ya *Fumo Liongo*. Haya yanabainika uk. 4 na uk 9 ambapo mtunzi ametumia lugha yenye muundo na mpangilio maalum wa mapigo na baadhi ya vina vinavyofanana mwishoni mwa mistari, ambavyo ni – "mbo" na" – "no". Tazama mfano ufuatao:

*WENA: Waziri Kiongozi: Maneno yako barabara, lakini huyu mtu si mtu, bali jini! Ukimnasa kwa ulimbo, atajinasua kwa fimbo tu, Ukimkomea kwa mambo atajikwamua kwa nyimbo tu, ukimng'ata kwa meno, yeye atajing'atua kwa maneno tu. Uk 4*

Chanzo: Data za Utafiti katika *Fumo Liongo* (Juni, 2022)

**Matumizi ya Nguvu za Sihiri**

Utafiti huu umebaini kuwa, nguvu za sihiri ni matini ambayo imetumiwa na msanii katika tamthiliya zote mbili. Katika *Ngoma ya Ng'wanamalundi* nguvu za sihiri zinajidhihirisha katika nguvu za kichawi na kiganga. Kwa mfano, mhusika Chidama amepewa nguvu za uchawi kama mbinu ya ukandamizaji na unyonyaji na kwa upande mwingine Ng'wanamalundi amepewa nguvu za uganga kama mbinu ya ukombozi na mapinduzi ya jamii ya wanyonge. Tazama dondoo namba 17 hapa chini:

*MELO: ...Ni pumzi za roho ngapi alizokwisha zinasa katika ile tunguri yake bwana wangu? Ebu: Toka mwezi juzi, kila siku kizuu mmoja. Wa kuvua samaki kumi. Wa kupalilia ishirini. Wa kuvuna mazao mbalimbali arobaini. Shughuli za nguruwe na kuku…* uk 10-11

Chanzo: Data za Utafiti (Juni, 2022)

Dondoo namba 17 hapo juu inadhihirisha matumizi ya mbinu ya nguvu za sihiri ambayo imetumika kisitiari kuwakilisha tabaka tawala na misingi ya unyonyaji, udhalimu, ukandamizaji na udhalilishaji inayotumiwa dhidi ya wananchi (vizuu).

Mbinu hii inajitokeza pia katika tamthiliya ya Fumo Liongo ambapo msanii ametumia mbinu ya sihiri kumchora mhusika Fumo Liongo. Amemchora kama ni mtu wa ajabu, mwenye nguvu za sihiri ambaye hawezi kufa kwa njia yoyote zaidi ya siri ya uhai na ufu wake ambayo ilikuwa iko kitovuni. Haya yanabainishwa uk.38 Zahidi akimweleza Mfalme Mringwari kuhusu maongezi yake na baba yake, Fumo Liongo. Kutokana na nguvu zake na miujiza yake, mitego anayotegwa huitegua na anafahamu kila kinachoendelea kumhusu yeye. Hali hii inasababisha waziri Wena kumwambia Waziri Kiongozi kuwa "maneno yako barabara lakini huyu si mtu, bali jini." uk 4. Watu walijenga imani kuwa Liongo si mtu wa kawaida bali ni jini. Miujiza iliyotokea siku ya kufa kwake nayo inakazia zaidi kuwa alikuwa na nguvu za ziada zitokanazo na ushirikina au mizimu. Haya

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1770

yanabainishwa uk. 44. Rejea mazungumzo ya Mwanamke 1 hadi 3.

Kwa mujibu wa Mulokozi (1996), sifa mojawapo ya shujaa chasili katika tendi za Kiafrika ni kuwa na nguvu za sihiri. Akiorodhesha sifa za shujaa chasili anasema, shujaa wa utendi anakuwa na sifa zifuatazo:

> *"-Nguvu. Hapa zinazungumziwa nguvu za kimwili yaani ubabe na mabavu nguvu za kiume na kidume, yaani urijali, nguvu za kiakili na nguvu za kivita.*
>
> *Uganga au nguvu za sihiri.*
>
> *Mshikamano na kundi au jumuiya*
>
> *Fulani inayomuunga mkono".* Uk 11

Chanzo: Data za utafiti katika *Tenzi Tatu za Kale* (Juni, 2015)

Mwingilianomatini unajitokeza katika matumizi ya nguvu za sihiri ambazo zinasadifu sifa za shujaa wa Kiafrika kama anavyosawiriwa kwenye fasihi simulizi za Kiafrika hususani ngano na visakale. Matumizi ya nguvu za sihiri pia ni matokeo ya athari ya utendi wa "Fumo Liongo" kwa mwandishi. Mwandishi anachota sifa za mhusika Fumo Liongo wa kwenye utendi na kuzihamishia kwenye tamthiliya ya *Fumo Liongo.*

Utafiti huu ulibaini kuwa, matumizi ya nguvu ya sihiri ni matokeo ya athari ya matumizi ya nguvu za sihiri yanayojitokeza katika utendi wa "Fumo Liongo". Mtunzi amechota vipengele na sifa zinazojitokeza katika utendi wa "Fumo Liongo" na kuzitumia katika kazi yake. Kristeva (1980) anafafanua mwingilianomatini kuwa sio urejelezi wa kazi fulani katika kazi nyingine tu, bali pia ni ule uingiliano wa mitindo ya kiuashiriaji. Hivyo mtunzi kwa kutumia sihiri kama mtindo na mbinu ya mwingilianomatini katika uashiriaji, ameweza kuibua masuala nyeti aliyokusudia kuyafikisha kwa hadhira.

**Mwingilianomatini ni Upekee wa Kimtindo wa Emmanuel Mbogo?**

Utafiti huu ulilenga kuchunguza iwapo matumizi ya mwingilianomatini ni upekee wa kimtindo wa utunzi wa Emmanuel Mbogo. Kupitia usomaji makini wa tamthiliya teule zote mbili na usaili kwa mtunzi, utafiti huu umebaini kuwa matumizi ya mwingilianomatini ni upekee wa kimtindo wa utunzi wa Emmanuel Mbogo. Hii ni kwa sababu matini zilizochunguzwa zimetumia mwongilianomatini kifani na kimaudhui. Data zinaonesha kuwa ingawa mtunzi alitunga matini hizi kwa kupishana muongo mmoja lakini hata baada ya muongo mmoja mtunzi ameendelea kufumbata mbinu ya mtindo wa matumizi ya mwingilianomatini katika utunzi wake. Hii inathibitisha kuwa utunzi wake umeathiriwa na mapokeo simulizi ya fasihi simulizi ya Kiafrika na anatumia mapokeo na masimulizi kama malighafi katika ubunifu na utunzi wa kazi zake za fasihi. Aidha, data za utafiti zinaonesha kuwa mapokeo ya masimulizi ya hadithi na visakale yamethibitishwa kumuathiri mtunzi kifani na kimaudhui kama yeye mwenyewe anavyothibitisha kuwa aliathiriwa na masimulizi na mpokeo hayo na kisha kuyaingiza katika ubunifu wa kisanii ili kutalii na kumulika uhalisia ulipo katika jamii. Jambo ambalo linaonekana kujidhihirisha katika muongo mmoja bila kubadilika.

Hata hivyo, utafiti huu ulibaini kuwa suala hili la mwingilianomatini linajitokeza sana katika kazi za Emmanuel Mbogo. Kwa mfano, ukichunguza tamthiliya zake za hivi karibuni utaona kuwa mtunzi ametawaliwa na mwingilianomatini katika utunzi wake. Hili linajidhihirisha katika vichwa vya tamthiliya zake ambazo zinaonekana kuwa zinatokana na masimulizi na matukio ya kweli mfano Nyerere na Safari ya Kaanani (2017), Bibi Titi Mohammed (2018) na Sadaka ya John OKero (2018) hizi zikiwa ni baadhi tu. Ukizisoma tamthiliya hizi utaona kuwa Emmanuel Mbogo hatungi tu kazi ya fasihi bali utunzi na ubunifu wake unachochewa na kuambatana na utafiti, ubunifu na athari ya masimulizi na uhalisia anaosimuliwa ama kushuhudia ndani ya jamii na

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1770

kisha kutumia masimulizi ama matukio hayo kutunga kazi zake za fasihi. Hivyo, makala haya yamebaini kuwa Emmanuel Mbogo amefumbata matumizi ya mwingilianomatini ambayo yanabeba na kuashiria upekee wa kimtindo wa utunzi wa Emmanuel Mbogo.

Utafiti huu pia ulibaini kuwa mtindo wa usanaji wa kazi za fasihi za Emmanuel Mbogo alizotunga kwa kupishana muongo mmoja unafanana. Mfanano huo unajidhihirisha katika matumizi ya mbinu za kimtindo zilizotumika kutunga tamthiliya hizo kama ambavyo imejadiliwa hapo awali. Tazama jedwali namba 2 hapa chini;

**Jedwali 2: Kufanana kwa Vipengele vya Kimtindo**

| Na. | Aina ya matini | Fumo Liongo | Ngoma ya Ng'wanamalundi |
|---|---|---|---|
| 1 | Ushairi | ✓ | ✓ |
| 2 | Nyimbo | ✓ | ✓ |
| 3 | Ngoma | ✓ | ✓ |
| 4 | Nguvu za Sihiri | ✓ | ✓ |
| 5 | Majigambo | ✓ | ✓ |

**Chanzo**: Data za Utafiti katika Matini Teule (Juni, 2022)

*Jedwali 2* hapo juu linaonesha kufanana kwa tamthiliya teule katika matumizi ya mbinu za kimtindo. Katika tamthiliya zote mtunzi ametumia mwingilianomatini kwa kutumia ngoma, nyimbo, majigambo, ushairi, na nguvu za sihiri kama mbinu ya kimtindo katika kuwasilisha maudhui yake.

Utafiti huu ulibaini kuwa mwandishi ametumia matini hizo ili kuingiza Uafrika katika utunzi wa tamthiliya teule, kuleta upya na mvuto wa kipekee katika ujumi wa tamthiliya hizo katika kutumia mazingira na fasihi simulizi ya Kiafrika. Aidha, sababu za kutumia matini hizo ni kwamba matini hizo ndizo zilizotumiwa katika matini za awali ambazo msanii alizipokea na hivyo msanii amezitumia kama na malighafi za kifani na kimaudhui katika kazi zake. Mbinu hii ya uchotaji na utumizi wa malighafi za kifani na kimadhui za matini tangulizi unaendana na nadharia ya Mwingilianomatini kuwa matini huzaliwa kutokana na matini iliyotangulia.

Vilevile, tamthiliya zote mbili ni matokeo ya athari ya masimulizi ya kimapokeo ya fasihi simulizi ya Kiafrika. Katika *Ngoma ya Ng'wanamalundi* mtunzi amethiriwa na masimulizi ya kisakale cha kabila la Wasukuma, kinachohusu habari za kweli za mtu maarufu katika kabila la Wasukuma aliyeitwa Mwanamalundi, aliyewahi kuishi mwaka 1892 hadi 1934. Kwa upande wa *Fumo Liongo* ni matokeo ya masimulizi ya utendi wa Kiafrika wa "Fumo Liongo" unaohusu habari za kweli za mtu shujaa na jasiri aliyeitwa Fumo Liongo, aliyeishi katika karne ya 13 hadi 14 katika mji wa Pate nchini Kenya. Uthibitisho wa athari hizo unajidhihirisha katika fani na maudhui ya tamthiliya hizo.

## HITIMISHO

Makala haya yalihusu matumizi ya mwingilianomatini kama upekee wa Emmanuel Mbogo. Data za makala haya zimedhihirisha kuwa mwingilinomatini ni upekee wa kimtindo wa Emmanuel Mbogo. Emmanuel Mbogo amejipambanua kimtindo kuwa ni mfuasi wa mwingilianomatini ambaye amejiegemeza katika matumizi ya mwingilianomatini katika utunzi wake. Hili linajidhihirisha katika matumizi ya mbinu za kimtindo za hadithi, ngoma, nyimbo, majigambo, wahusika wa fasihi simulizi, ushairi na nguvu za sihiri. Hivyo, makala haya yanahitimisha kuwa kila mtunzi ana upekee wake katika utunzi na uandishi wa kazi za fasihi, upekee huu huweza kuonekana katika uteuzi wa mtindo wa uandishi ambao unajirudiarudia katika kazi zake. Hii inathibitishwa na mbinu ya mwingilianomatini ilivyojitokeza katika tamthiliya zote mbili, ingawa zimetungwa na mtunzi katika vipindi tofauti vilivyopishana kwa takribani muongo mmoja. Lakini bado ilionekana kuwa malighafi, mbinu, mtindo na mawazo ya utunzi wa kazi hizo ni yaleyale. Hii

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1770

inatuthibitishia kuwa, mtunzi ameendelea kufumbata mbinu ya mwingilianomatini katika utunzi wake, na huu ndio mtindo wake wa utunzi wa kazi za fasihi. Vile vile makala haya yamejadili kuwa, mtunzi huingiza mbinu za ubunifu wa kimtindo katika kuwasilisha mapokeo aliyoyapata ili kuibua dhamira mbalimbali ndani ya jamii. Hivyo, mtunzi hatungi kazi zake nje ya jamii, mazingira yake na muktadha wa jamii yake. Kwa mantiki hiyo, Makala haya yanahitimisha kuwa matumizi ya mwingilianomatini ni upekee wa kimtindo wa Emmanuel Mbogo katika utunzi wa kazi za fasihi ambao ulijidhihirisha ndani ya mwongo mmoja. Hata hivyo, Makala haya yanapendekeza kuwa bado kuna haja ya kuthibitisha upekee wa kimtindo wa Emmanuel Mbogo kupitia kazi zake za miaka ya 2000 kupitia tafiti.

**MAREJELEO**


Allen, G. (2000). *Intertextuality*, Routledge, London.

Bakhtin, M.M. (1984). *Problems of Dostoevskys Poetics*, Minneapolis: University of Minnesota Press.

Boaz, B. Z. (1974). Mwanamalundi: Mtu Maarufu katika Historia ya Usukuma, Wizara ya Elimu ya Taifa, Dar es Salaam, Tanzania

Fairclough, N. (1992). *Discourse and Social change*. Cambridge: Polity press.

Herman, L. (2011). Dhana ya Mwingilianomatini kwenye Hadithi za Watoto katika Kiswahili, *Kioo cha Lugha*: Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kristeva (1969). *Desire in Language: A Semiotic Approach to Literature and Art*. Translated by

Leon Roudiez. New York: Columbia University Press,

Kristeva, J. (1980). Desire in Language: A Semiotic Approach to Literature and Art, Columbia University Press, New York.

Kristeva, J. (1984). Revolution in Poetic Language. (Trans. Margaret Waller, Intr. Leon S. Roudiez), Columbia UP, New York. 325 M. Zengin

Kristeva, J. (1986). The Kristeva Reader. (Ed. Toril Moi), Columbia University Press, New York.

Lemanster, T. (2012). What is intertextuality, Great World Text: A programme of the Centre for Humanities, University of Wisconsin- Madson, Wisconsin.

Mbogo, E. (2009). *Fumo Liongo*, Dar es Salaam University Press, Dar es Salaam.

Mbogo, E. (1988), *Ngoma ya Ng'wanamalundi*, Education Services Centre Ltd, Dar es Salaam

Macha, N (2013). Matumizi ya mtindo wa Mwingilianomatini

Moi, T. (1986). Introduction; The Kristeva Reader, Columbia University Press, New York.

Mulokozi, M. M (1996). *Fasihi ya Kiswahili*, Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania, Dar es Salaam.

Mutembei, K.A. (2012). *Korasi katika Kiswahili: Nadharia mpya ya Uhakiki*, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam.

Mningo, R. (2015). Thathmini ya Mwingilianomatini katika Utunzi wa Emmanuel Mbogo: Utafiti Linganishi wa Tamthiliya ya Ngoma ya Ng'wanamalundi na Fumo Liongo. Tasnifu ya MA. Kiswahili. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Dar es salaa,

Samwel, M. (2012) *Hadithi Fupi: Nadharia, Mbinu na Mifano*, Dar es Salaam: Kasenyenda Tanzania

Senkoro, F.E.M.K (2011). *Fasihi: Mfululizo wa Lugha na Fasihi*, KAUTTU, Dar es Salaam.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1770

TUKI. (1999). Tenzi Tatu za Kale: Fumo Liongo, Al – Inkishafi, Mwanakupona, Taasisi Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania

TUKI, (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (toleo la 3) Oxford University Press, Nairobi.

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele vyake*, Phoenix Publishers Ltd, Nairobi

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi Fasihi: Istalahi na Nadharia*, Focus Publication Ltd, Nairobi, Kenya.

Wamitila, K.W. (2008). Kanzi ya *Fasihi: Misingi na Uchambuzi wa Fasihi*, Daisy Printers (K) Ltd, Nairobi, Kenya.

Worton, M. & Still, J. (1990). Introduction, Intertextuality: Theories and Practices, Manchester UP, Manchester and New York, pp. 1-44.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.